Jina……………………………………………………………………….. Nambari Yako………………..

102/2 Sahihi ………………………….
KISWAHILI
Karatasi ya 2 Tarehe…………………………
(LUGHA)
Julai/Agosti 2014
Muda: Saa: 2½

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

# MTIHANI WA MWIGO WA CEKENA KIDATO CHA NNE – 2014

**Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 2**
**(LUGHA)**
**Muda: Saa: 2½**

**MAAGIZO:**

1. Karatasi hii ina maswali manne (Ufahamu, Ufupisho, Lugha na Isimu Jamii).
2. Jibu maswali yote kwenye nafasi zilizoachwa baada ya kila swali.

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| | SWALI | UPEO | Alama |
|---|---|---|---|
| 1 | Ufahamu | 15 | |
| 2 | Ufupisho | 15 | |
| 3 | Matumizi ya Lugha | 40 | |
| 4 | Isimu Jamii | 10 | |
| | JUMLA | 80 | |

1. **SEHEMU A: UFAHAMU (ALAMA 15)**

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.**

For More Free KCSE Past Papers Visit www.freekcsepastpapers.com

Ushauri na uelekezaji ni mojawapo ya mikakati ambayo inatumiwa na taasisi na mashirika mengi katika kurekebisha tabia. Msimamo wa kijadi kuwa adhabu kali ndiyo njia mufti ya kumshinikiza binadamu kuacha mienendo hasi unaendelea kufifia na mahali pake kutwaliwa na nasaha na ushawishi. Hata katika mazingira magumu kama gerezani, ushauri na uelekezaji umeonekana kuzaa matunda kwa kuwasaidia wafungwa kubadili mienendo hasi na kukabiliana na makali ya matendo yao.

Kila mwanajamii, wazee kwa vijana, wake kwa waume, wenye furaha kwa wenye majonzi huhitaji nasaha. Nasaha humwezesha mtu kustahimili hali ngumu katika maisha. Wanaougua magonjwa sugu kama vile iri huhitaji ushauri ili kuishi kwa mitazamo chanya na kupunguza makali ya unyanyapaa na hali ya kujihurumia inayotokana na maradhi hayo.

Halikadhalika, binadamu huhitaji mawaidha wakati anapovuka kutoka daraja moja la maisha hadi jingine. Kila awamu katika maisha ya binadamu huwa na changamoto, majukumu na matarajio yake. Maarusi, kwa mfano, huhitaji nasaha ya kuwawezesha kukabiliana na changamoto za ndoa. Aidha vijana wanaotiwa jandoni hihitaji ushauri wa kuwasaidia kuyamudu majukumu ya utuuzima. Si ajabu kuwa tangu jadi manyakanga wamekuwa wakiwausia wanaotiwa jandoni kuhusu kunga za utuuzima.

Ingawa kila mwanajamii anahitaji ushauri na uelekezaji, vijana ndio wanaouhitaji zaidi kwa sababu hawana uzoefu mpana wa maisha. Vijana wanaohitimu masomo ya shule za upili, kwa mfano, wanahitaji kuelekezwa kuhusu taaluma katika vyuo vikuu, umuhima na mahitaji ya taaluma hizo. Isitoshe, wakati wa kukfanya mitihani vijana huhitaji nasaha.

Mazingira ya binadamu hubadilika, nayo maisha yake hutwaa mabadiliko yanayotokana na hali mpya. Baadhi ya watu wanapojipata katika mazingira mageni wasiyoyaweza, hupatwa na woga au unyonge Fulani ambao huenda ukawaathiri. Wengine, pengine kwa sababu ya maisha duni ya awali, huweza kuathiriwa na kujiona kuwa wenye thamani ya chini wakijilinganisha na wenzao. Kuna wanafunzi au hata wafanyikazi ambao kwa sababu ya kutofikia malengo yao shuleni au kazini, hufa moyo na hata kutaka kuiacha shule au kazi hiyo. Watu kama hawa huhitaji nasaha ili wajikubali jinsi walivyo na hata waweze kutumia udhaifu wao kuboresha maisha yao ya usoni.

Wengi hudhani kuwa wanaohitaji nasaha ni wale wenye matatizo tu. Ukweli ni kwamba, hata wale ambao wanaonekana kuwa na furaha na vyeo wanahitaji ushauri wa aina Fulani. Wenye mali, kwa mfano, wanaweza kushauriwa kuhusu namna ya kuwekeza ili wasifilisike. Viongozi nao wanahitaji nasaha ili waandame sera bora za uongozi pamoja na jinsi ya kuishi kwa mwamana na wanajamii wenzao.

Ushauri na uelekezaji, kwa hakika, unahitajika katika nyanja zote za maisha. Ni muhimu kukumbuka kuwa ushauri huanzia nyumbani. Mzazi au mlezi ndiye mshauri wa kwanza. Haifai wazazi kuchelea kuwashauri watoto wao mapema, kwa maana mchelea mwana kulia hulia mwenyewe.

Maswali

1. Ipe taarifa hii anwani mwafaka. (alama 1)

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

2. Tofautisha urekebishaji tabia wa kijadi na wa kisasa. (alama 2)

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

3. Taja mazingira yoyote manne ambapo binadamu huhitaji nasaha na uelekezaji. (alama 4)

4. Eleza umuhimu wa kushauri watu wafuatao:
(a) Viongozi. (alama 2)

(b) Wenye mali.

5. Wazazi wasiowausia watoto wao wataathirika vipi hatimaye? (alama 2)

6. Andika methali yoyote inayohusiana na nasaha. (alama 1)

7. Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika taarifa: (alama 3)
(i) Unyanyapaa.

(ii) Manyakanga

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

(iii) Mitazamo chanya.

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

2. **MUHTASARI.**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu.**

Kiswahili ni lugha yenye asili yake katika ukanda wa Afrika Mashariki. Imeenea kote duniani ambako inafundishwa katika vyuo vikuu saba vya umma na vyuo vikuu viwili visivyo vya umma. Hivi ni Baratoni na Chuo Kikuu cha Kikatoliki. Katika kiwango hiki, watu wanafunzwa isimu na fasihi. Mafunzo haya yanatolewa kuanzia shahada ya kwanza, shahada ya uzamili na shahada ya uzamifu.

Elimu ya juu ya Kiswahili inatiliwa mkazo katika vyo vikuu nchini Tanzania na hasa Dar-es-Salaam. Chuo hiki ndicho mlezi wa Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI). Kwa muda mrefu, TUKI imechapisha majarida, kuzua istilahi na kuandaa kamusi. Vyuo vikuu nchini Uganda vikiongozwa na Makerere vimeanzisha mikakati kabambe ya kufunza Kiswahili. Kwingineko barani Afrika, Kiswahili kinafunzwa nchini Msumbiji, Sudan, Misri, Lesotho, Ghana, Nigeria na kadhalika. Lugha hii imepewa msisimko mkubwa katika mitaala kuambatana na sera ya Afrika Kusini kutukuza lugha za Kiafrika. Ikumbukwe kuwa lugha hii ilichangia pakubwa ukombozi wa Afrika Kusini.

Ukitembelea baadhi ya vyuo vikuu katika nchi za mashariki ya mbali kama Japani, Korea Kusini na Uchina, utapata Kiswahili kwenye orodha ya masomo. Maandishi mengi yanatafsiriwa kwa Kiswahili katika vyuo hivi. Takribani nchi zote Ulaya zina vyuo vikuu vinavyofunza Kiswahili. Lakini Uingereza, Ujerumani na nchi za Skandinevia zimetia fora. pamoja na kufunza lugha hii, vyuo vinafadhili utafiti na uchapishaji wa mambo kuhusu Kiswahili. Aidha, nchi hizo huwadhamini wengi kusomea huko. Muhimu zaidi ni kuwa vyuo vikuu katika nchi hizo zimehifadhi maandishi mengi ya Kiswahili. Hivi sasa wasomi wengi wanayatumia kufanya utafiti hasa kuhusu ushairi. Moja ya asasi hizi ni School or Oriental and African Studies, jijini London. Wataalamu waliosomea vyuo hivi wamerudi nyumbani na sasa wanajihusisha na uchapishaji wa vitabu vya nadharia, isimu, sarufi, fasihi andishi na fasihi simulizi.

Hata hivyo, ni Marekani ambapo matumizi na mafunzo ya Kiswahili katika vyuo vikuu yamepanuka sana. Lugha hii inafunzwa katika majimbo kama Washington, NewYork, Chicaho, Texas, California, New Jersey na kadhalika. Vyuo maarufu sana kama vile Cornel, Yale na Havard vinafunza Kiswahili. Hali hii imesaidia kuingizwa kwa lugha hii katika mtandao.

Lugha hii inafunzwa kama ishara ya hisia za uafrika. Wamarekani weusi wanaona fahari kuzungumza Kiswahili. Hii huwakumbusha kuwa wao wana asili yao barani Afrika. Kupitia mafunzo haya, Wamarekani wengi wanaiga utamaduni wa Kiafrika. Wengi wao wamejipa majina ya Kiswahili kama vile Baruti, Katembo, Maulana, Simba na kadhalika. Kwa hakika Kiswahili kinapata hadhi.

*Maswali:*

(a) Bila kupoteza maana iliyokusudiwa na mwandishi, fupisha aya ya kwanza na aya ya pili.
**(Maneno 50-60)** **(alama 6, 1 ya Mtiririko)**

**Matayarisho**

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

**Jibu**

(b) Kwa kuzingatia aya tatu za mwisho, eleza mambo muhimu anayoyaeleza mwandishi kuhusu ufundishaji wa Kiswahili katika vyuo vikuu. **(Maneno 60 – 70)** **(alama 9, 1 ya Mtiririko)**

**Matayarisho**

**Jibu**

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

3. **MATUMIZI YA LUGHA:**

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

(a) Eleza dhana ya ala za sauti. (alama 2)

(b) Eleza kwa nini /y/ na /w/ huitwa nusu irabu. (alama 1)

(c) Eleza neno mojamoja lenye muundo wa silabi zifuatazo: (alama 2)

(i) Silabi funge -

(ii) Irabu pamoja na konsonanti (IK) -

(iii) Silabi huru -

(iv) Silabi mwambatano -

(d) Taja ngeli za nomino zifuatazo: (alama 2)

(i) Ngisi -

(ii) Kiu -

(e) Weka shadda katika kitenzi kwenye sentensi ifuatayo. (alama 1)

Paka yu juu ya mti.

(f) Tambua kiima, shamirisho, chagizo na kiarifu katika sentensi ifuatayo: (alama 4)

Nyanya alimjengea mjukuu nyumba kwa matofali mwaka jana.

(g) Tunga sentensi moja kudhihirisha maana ya vitate hivi. (alama 1)

Afya na Avya

_______________

_______________

(h) Ainisha viambishi katika neno “kulibomolewa”. (alama 2)

(i) Kimuundo

_______________

_______________

(ii) Kimajukumu

_______________

_______________

(i) Andika katika kauli ya kutendesha. (alama 2)

Alikufa kwa sababu ya ugonjwa wa kipindupindu.

_______________

_______________

(j) Eleza maana **mbili** za sentensi ifuatayo: (alama 2)

Mtoto anapendezwa na ziwa.

_______________

_______________

(k) Tumia neno ‘udhalimu’ katika sentensi kama: (alama 2)

(a) Kivumishi

_______________

_______________

(b) Kitenzi

_______________

_______________

For More Free KCSE Past papers visit www.freekcsepastpapers.com

(l) Andika sentensi ifuatayo katika **ukubwa** hali ya **wingi**: (alama 2)

Mwanafunzi alikwaruzwa uso na kiti kilichokuwa kando ya mti uliokuwa karibu na nyumba yao.

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

(m) Bainisha vishazi katika sentensi ifuatayo: (alama 2)

Ningesoma kwa bidii ningepita mtihani.

(n) Pambanua sentensi ifuatayo kwa kutumia mishale/mistari. (alama 4)

Wanafunzi waliopita mtihani walichinjiwa nguruwe mnono sana.

(o) Tunga sentensi moja kudhirihisha matumizi **mawili** tofauti ya **'po'**. (alama 2)

(p) Akifisha sentensi ifuatayo.

je umewahi kusoma kitabu cha nyota ya rehema aliuliza. (alama 4)

(q) Ainisha sentensi ifuatayo kimuundo na kimajukumu. (alama 2)

Someni kwa bidii.

(r) Taja nahau yenye maana sawa na 'jifunge masombo'. (alama 1)

(s) Eleza ni kwa nini neno 'umma' ni la asili ya kigeni. (alama 1)

(t) Ngeli ni nini? (alama 1)

4. **ISIMU JAMII**

1. Eleza maana ya viziada lugha. (alama 2)

2. Fafanua sababu **nne** zinazomfanya mtu kutumia viziada lugha anapozungumza. (alama 8)

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com